



Sungura alikuwa amelala chini ya mtofaa. Tofaa lilianguka chini kutoka tawi moja.



Sungura aliisikia sauti ikisema, 'Kimbia, Sungura, kimbia!' Sungura aliamka na bila kukawia akaanza kukimbia mbio sana.




Sungura alikutana na Kuku. "Mbona unakimbia?" Kuku alimwuliza. Sungura akamjibu, "Sijui. Nilisikia tu kitu kikianguka nayo sauti ikasema, 'Kimbia, Sungura kimbia!'"



Kuku alishituka akaanza
kukimbia alipomsikia
maneno aliyosema
Sungura.



Walikutana na Mbwa akawauliza, “Kwa nini mnakimbia?” Kuku akamjibu, “Sijui. Nilisikia Sungura akipiga makelele naye hajui. Alisikia kitu kikianguka na sauti ikisema, 'Kimbia, Sungura kimbia!'”



Mbwa akashangaa akaanza
kukimbia pamoja na
Sungura na Kuku.



Walikutana na Farasi
akawamwuliza Mbwa,
“Mbona mnakimbia?”
Mbwa akamjibu, “Sijui.
Nilisikia Kuku akisema hajui
na wala Sungura hajui.
Alisikia kitu kikianguka na
sauti ikisema, 'Kimbia,
Sungura kimbia!’”



Farasi naye akaanza
kukimbia pamoja na
Sungura, Mbwa na Kuku.



Walikutana na Punda akawauliza, “Kwa nini mnakimbia?” Farasi alimjibu, “Sijui. Nilimsikia Mbwa akisema hajui. Yeye alimsikia Kuku ambaye hajui. Kuku naye alimsikia Sungura ambaye pia hajui. Alisikia tu kitu kikianguka na sauti ikisema, 'Kimbia, Sungura, kimbia!'”



Basi Punda pia akaanza kukimbia pamoja na Sungura, Mbwa, Kuku na Farasi.




Walikutana na Ng'ombe akawauliza, "Kwa nini mnakimbia?" Punda alimjibu, "Sijui. Nilisikia alivyosema Farasi, naye hajui. Yeye alisikia Mbwa na Mbwa hajui. Alimsikia Kuku naye Kuku hajui. Alimsikia Sungura naye pia hajui. Yeye alisikia kitu kikianguka na sauti ikisema, 'Kimbia, Sungura, kimbia!'"



Ng'ombe akapata wasiwasi
na akaanza kukimbia
pamoja na Sungura, Mbwa,
Kuku, Farasi na Punda.



Walikutana na Paka akauliza, “Kwa nini mnakimbia?” Ng'ombe alijibu, “Sijui. Nilisikia tu alivyosema Punda naye hajui. Yeye alimsikia Farasi naye Farasi hajui. Alimsikia Mbwa ambaye hajui. Yeye alimsikia Kuku na Kuku hajui. Kuku alimsikia Sungura ambaye hajui ila alisikia kitu kikianguka na sauti ikisema, 'Kimbia, Sungura, kimbia!'”



Paka naye akaanza kukimbia pamoja na wanyama wengine.



Walikutana na mvulana aliyekuwa amepanda baiskeli. Mvulana aliwauliza, "Mbona nyote mnakimbia?" Wanyama walimjibu, "Hatujui. Tulimsikia Sungura alivyosema naye hajui. Alisikia kitu kikianguka na sauti ikisema, 'Kimbia, Sungura, kimbia!'"



Mvulana alicheka akasema,
“Upepo uliangusha tofaa.
Mimi ndiye nilisema,
'Kimbia, Sungura kimbia!'”